# KISTE EXAMINATION PANEL

## DARASA LA SABA – 007

## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

**Som vifungu vifuatavyo. Vina nafasi kutoka nambari 1 hadi 15. Kwa kila nafasi, chagua jibu sahihi kati ya yale uliyopewa**

Babu Tandatu ___1___ sisi sote. Mara kwa mara, alitupa mawaidha ambayo yalitusaidia maishani kwani yeye ___2___ alikuwa ameyaona mengi. Tulipokuwa na jambo ambalo lilitutinga akili, hatukuchelea kusaili kutoka kwake ili tujue mengi. Naam, ___3___. Naye babu alifurahia sana kukaa nasi wajukuu wake na kutufunza mengi. Kila jioni baada ya ___4___, sote tulikuwa tukienda chumbani mwake babu kwa nia ya kuzisikiliza hadithi zake tamu. Ni nani asiyejua kuwa maneno matamu ___5___ ?

Jioni moja, babu alikuwa akiota moto nje ya chumba chake. Kama ___6___ desturi, tulijiunga naye. Sote tulitulia tuli na kutega masikio ___7___ ! Baada ya kuongea machache ndipo alipotueleza jinsi watoto na watu wazima kwa jumla ___8___ wakati wao kwa kufanya mambo yasiyofaa. "Kutopanga wakati wenu vizuri kutawafanya mtende maovu," babu ___9___.

1. A. aliwapenda B. alitupenda C. alimpenda D. alinipenda
2. A. mwenyewe B. wenyewe C. yenyewe D. lenyewe
3. A. udongo uwahi uli maji B. chema chajiuza kibaya chajitembeza C. msafiri ni aliye bandarini D. kuuliza si ujinga
4. A. kisebeho B. chamcha C. chajio D. kishuka
5. A. humtoa nyoka pangoni B. humrudisha mwana tumboni C. hujenga badala ya kubomoa D. hujaa hila na hadaa
6. A. ilipokuwa B. ilivyokuwa C. iliyokuwa D. inapokuwa
7. A. ti B. nda C. ndi D. twa
8. A. wanavyolipoteza B. wanavyoipoteza C. wanapoupoteza D. wanavyoupoteza
9. A. alitushurutisha B. alitushauri C. alituuliza D. alisaili

Hatua ya mwisho baada ya mwanafunzi kusoma kipengele ___10___ cha somo la Kiswahili ni kupima ufahamu wake wa yale yote aliyosoma. Mara nyingi, anaweza akajibu maswali mbalimbali kimoyomoyo ___11___ wakati ___12___ anaweza kufanya mazoezi kwa kuandika majibu ya maswali mbalimbali. Endapo maswali ___13___ ni magumu na yamemlemea, mwanafunzi anapaswa kutafuta maelezo kutoka kwa mwalimu wake. ___14___ kuelewa, ni vyema mwanafunzi awe akidurusu ___15___ ili asisahau.

10. A. chochote B. yoyote C. lolote D. zozote
11. A. labda B. alimradi C. ilhali D. lahaula
12. A. nyingine B. mingine C. wengine D. mwingine
13. A. yayo huyo B. yayo hayo C. hizo hizo D. hayo yayo
14. A. Kabla ya B. Kati ya D. Baadhi ya D. Baada ya
15. A. hobelahobela B. kovoloya C. mara kwa mara D. shaghalabaghala



PRINTED BY KISTE PRINTERS

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu kila swali kulingana na maagizo***

16. Chagua wingi wa sentensi ifuatayo:
Baharia yule alimnasa mjusi mkubwa
A. Mabaharia wale waliwanasa mijusi wakubwa
B. Mabaharia wale waliwanasa wajusi wakubwa
C. Baharia wale waliwanasa mijusi wakubwa
D. Baharia hawa waliwanasa mjusi mkubwa

17. **Bainisha sentensi ambayo imeandikwa katika hali timilifu.**
**A. Yeye hututembelea kila siku ya Jumapili.**
B. Akiamka mapema atasafiri kwa gari la moshi.
C. Alienda sokoni kununua mboga na matunda.
D. Wimbo mzuri umeimbwa na mtoto.

18. Chagua orodha ambayo ina vivumishi viashiria pekee.
A. Hodari, kamili, lufufu, gani
B. Wale, zile, humo, hivyo
C. Wengi, wote, tano, kidogo
D. Mbona, lini, mimi, ngapi

19. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.
Babu aling'oa nanga macheo.
A. Bibi alitia nanga machweo
B. Babu alitia nanga machweo.
C. Nyanya alitia nanga Mashariki.
D. Nyanya aling'oa nanga Magharibi.

20. Bainisha matumizi ya 'kwa' katika sentensi ifuatayo:
Mwalimu alimtazama mwanafunzi kwa dharau
A. Kuonyesha kihusishi
B. Kuonyesha idadi
C. Kuonyesha namna
D. Kuonyesha nia

21. Chagua ukubwa na wingi wa sentensi ifuatayo:
Mlango wa chumba hicho umefunguliwa.
A. Lango la jumba hilo limefunguliwa.
B. Malango ya majumba hayo yamefunguliwa.
C. Milango ya vyumba hivyo imefunguliwa.
D. Vilango vya vyumba hivyo vimefunguliwa.

22. Akisami $^{3}/_{5}$ huitwa:
A. thuluthi B. khumusi thuluthi
C. tatu tano D. khumusi tatu

23. Unganisha sentensi zifuatazo kwa usahihi:
Maria alichelewa kufika shuleni. Aliamba mapema.
A. Maria alichelewa kufika shuleni kwani aliamba mapema.
B. Ingawa Maria aliamka mapema, alichelewa kufika shuleni.
C. Maria aliamka mapema aidha alichelewa kufika shuleni.
D. Maria alichelewa kufika shuleni maadamu aliamka mapema.

24. Tunasema msiri kama kaburi, aidha, pendeza kama
A. hurulaini B. kipepeo
C. bafta D. halua

25. Kikuku ni pambo ambalo huvaliwa
A. shingoni B. sikioni
C. mkononi D. kiunoni

26. Chagua semi inayosimamia maelezo yafuatayo:
Kutoa maneno yaliyokukaa moyoni, hasa mazito.
A. Jipiga kifua B. Tokwa na ulimi
C. Pasua mbarika D. Jikuna kichwa

27. Geuza sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa:
Mwalimu wa Kiswahili alipiga simu.
A. Mwalimu wa Kiswahili alipigisha simu
B. Mwalimu wa Kiswahili alipigiwa simu
C. Mwalimu wa Kiswahili alipigishwa simu.
D. Mwalimu wa Kiswahili alipigiana simu

28. Chagua kisawe cha methali ifuatayo:
Damu ni nzito kuliko maji.
A. Usitukane mamba kabla ya kuvuka mto
B. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi
C. Tamaa mbele mauti nyuma
D. Ndugu mui heri kuwa naye.

29. Msimamizi mkuu wa mabaharia huitwa
A. sarahangi B. nahodha
C. mkadamu D. nokoa

30. Sungura ni kwa kibuyu kama vile papa ni kwa
A. kiyoyo B. king'onyo
C. Kinengwe D. kivinimbi

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 – 40***

Rehema alikuwa mrembo aliyeumbwa akaumbika. Alikuwa mwana wa pekee wa Bwana na Bi. Mapesa. Walikuwa wakwasi tajika ambao walisifika kote kijijini kutokana na ukwasi wao ambao ulianzia kwenye mashamba yao makubwa, mifugo yao nyingi kampuni mbalimbali na pesa zilizokuwa nyingi mithili ya mchanga wa baharini. Kila uchao, adinasi wengi pale kijijini walienda nyumbani kwake Bwana Mapesa kuomba kazi yoyote ya kibarua ili angalau mkono uende mdomoni. Ingawa kazi walizopewa zilikuwa kazi za kijungu jiko, hawakujali kwani lisilo na budi hubidi.

Bwana na Bi Mapesa walimtunza mwanao kama dhahabu. Hakuna alichokosa kwani alikidhiwa mahitaji yake yote. alichokosa basi hakikupatikana madukani. Walimdekeza na kumuonyesha raha za

dunia bila kujua ya kuwa mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Alipofikisha umri wa kuenda shuleni, Rehema alipelewa katika mojawapo wa shule tajika nchini ambazo zilikuwa za walalaheri tu. Maskini walipata kujua habari zake kwenye magazeti. Walimu wote waliuma uzi kumfunza Rehema mambo yote ambayo yalifunzwa shuleni. Aidha, babake aliwaajiri walimu wa ziada wa kumfunza nyumbani baada ya shule na pia wakati wa likizo. Hata hivyo, Rehema alikuwa kisu butu. Masomo kwake yalikuwa ni kama maji na mafuta. Hawakutangamana.

Isitoshe, Rehema alianza kuwa na tabia za mkia wa mbuzi. Mara nyingi, aliwakosea heshima walimu pamoja na wanafunzi wenzake. Aliwaona kuwa watu duni kwani hakuna yule aliyetoka familia tajiri kama yeye. Hakujua kuwa mpanda ngazi hushuka, aidha mbio za sakafuni huishia ukingoni. Walimu walijaribu kumpa ushauri nasaha lakini maneno yao yaliangukia masikio yaliyotiwa nta. Rehema hakuwa tayari kusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Basi walimu walivyoona hivyo, walitupa jongoo na mti wake huku wakimuonya kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Alipojiunga na shule ya upili, mwenendo ulikuwa ni huo huo. Rehema alizidi kuwa mtovu wa nidhamu huku mara nyigi akitoroka bwenini usiku na kuenda kubugia vileo kwenye vilabu vilivyokuwa karibu. Wanafunzi wengi hawakutaka kujihusisha naye kwani hawakutaka kuambukizwa tabia za utovu wa nidhamu. Walitengana naye kama vile ardhi na mbingu. Alipofika kidato cha tatu, Rehema alishindwa kuendelea na masomp. Alitoroka shuleni na kuhamia mjini ambako aliendelza tabia yake ya kubugia pombe na kuhudhuria vilabu kwa minajili ya kushiriki sherehe na kujiburudisha.

Baada ya miaka michache, wazazi wake walimrai Rehema kurudi nyumbani lakini hawakufua dafu. Rehema alizamia lulu mjini. Hakuona maana ya kurudi mashambani. Hatimaye, Rehema alianza kuwa na senene ambazo hazikuisha. Alikonda na kukondeana kama ng'onda. Alipoenda hospitalini, iligunduliwa kuwa alikuwa na ugonjwa ambao haukuwa na tiba. Marafiki aliokuwa nao walimtoroka na kumtenga kama mgonjwa wa ukoma. Hapo ndipo Rehema alipoamua kuwarudia wavyele wake, japo kwa tahayuri kuu. Aliwaelezea habari za kugonjeka kwake kwa huzuni, nao wazazi wakatiririkwa na machozi njia mbili mbili. Hawakuwa na budi kuyapokea matukio hayo makuu kwani maji yakimwagika hayazoleki.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, si sahihi kuwa
A. wazazi wake Rehema walikuwa watu wenye vyao
B. Rehema alikuwa mwanambee katika familia ya watoto wanne
C. wanakijiji walienda nyumbani kwa Bwana Mapesa kutafuta vibarua
D. Bwana na Bi. Mapesa walikuwa watu waliosifika kijijini

**32.** Kinyume cha neno 'mrembo' kama lilivyotumika katika taarifa ni
A. banati B. mtwana
C. mtanashati D. barobaro

**33.** Maana ya semi 'kazi za kijungu jiko' katika taarifa ni
A. kazi ambazo zinachosha sana
B. kazi zenye mapato madogo sana
C. kazi za kulazimishwa
D. kazi za kinyumbani

**34.** Ni nini kinachoonyesha kuwa Bwana na Bi. Mapesa walimdhamini mwanao?
A. Alikuwa mwana wao wa pekee
B. Alizaliwa katika familia ya walalaheri
C. Aliuma uzi katika masomo yake
D. Walimkidhia mahitaji yao yote

**35.** Si kweli kusema kuwa Rehema
A. alipelekwa katika shule isiyokuwa na hadhi
B. hakuwa mwepesi wa kuyaelewa masomo yake
C. aliwadharau walimu na wanafunzi wengine
D. alikuwa mwenye kiburi na mtukutu

**36.** Kwa nini Rehema aliwakosea heshima watu wengine?
A. Wazazi wake hawakumfunza umuhimu wa heshima
B. Hawakutoka katika familia zenye ukwasi kama yeye
C. Alikuwa mwepesi wa kuyaelewa mambo
D. Walimu na wanafunzi wenzake walimdharau

**37.** **'Wanafunzi wengi hawakutaka kujihusisha naye kwani hawakutaka kuambukizwa tabia za utovu wa nidhamu.'** Chagua methali inayoweza kusimamia maneno haya
A. Mui huwa mwema
B. Fimbo ya mbali haiui nyoka
C. Nazi mbovu harabu ya nzima
D. Joka la mdimu huwalinda watundao

**38.** Si kweli kuwa baada ya Rehema kugonjeka
A. alizidi kukonda na kuwa hafifu
B. aliamua kurudi nyumbani kwa wavyele wake
C. alitorokwa na kutengwa na wasena wa karibu
D. marafiki zake walimtembelea na kumpa pole

**39.** Neno 'tahayuri' kama lilivyotumika katika taarifa lina maana sawa na
A. ghadhabu B. soni
C. huzuni D. majonzi

**40.** Chagua mada ifaayo taarifa hii bora zaidi.
A. Mchumia juani hulia kivulini
B. Baada ya dhiki ni faraja
C. Mpanda ngazi hushuka
D. Chako ni chako chetu si chako

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 – 50**

Haki za watoto duniani ni anuwai. Kila taifa kote ulimwenguni limeifa kipaumbele suala la haki za watoto. Je, mtoto ni nani? Mtoto ni mtu yeyote aliye na umri wa chini ya miaka kumi na minane. Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha sana kuwa watoto bado wanazidi kudhulumiwa kwa njia mbalimbali licha ya kuwepo na sheria nyingi zilizoundwa ili kulinda haki zao. Jambo la kulinda watoto pamoja na haki zao linapaswa kuvaliwa njuga la sivyo, kizazi cha kesho, ambacho huundwa na watoto wa leo, huenda kikaangamia.

Mojawapo ya haki za watoto ni haki ya kupata elimu. Kila mtoto anapaswa kupelekwa shuleni ili kupata elimu. Hata hivyo, watoto wengi, hasa katika mataifa ambayo hayajaendelea, hawaendi shuleni. Jambo hili huchangiwa zaidi na hali ya umaskini uliokithiri. Badala ya kuenda shuleni, watoto wengi hujiunga na wazazi wao katafuta riziki. Katika mataifa ya aina hii, elimu huonekana kama tunu iliyotengewa wateule, yaani watu walio na vyao. Lakini, hali haipaswi kuwa hivi. Elimu ni kitu ambacho kila mtoto kote duniani anapaswa kupata, awe ametoka katika familia maskini ama tajiri.

Aidha, watoto wana haki ya kulindwa dhidi ya dhuluma na mateso. Kuna njia nyingi ambazo hutumiwa kuwadhulumu watoto. Kwa mfano, watoto hudhulumiwa pale wanapobakwa. Ubakaji umekithiri zaidi katika jamii. La ajabu ni kuwa, watu wanaowabaka watoto ni wale ambao wanastahili kuwa katika mstari wa mbele kuwalinda. Watoto wanapobakwa, wao huvunjiwa ubikira wao. Hiki ni kitendo cha kinyama sana na wanaokitekeleza wanapaswa kutiwa mbaroni na <u>kula kalenda</u> aushi yao yote. Isitoshe, kuna baadhi ya mabwanyenye ambao huwaajiri watoto kama vitwana au vijakazi. Wao hawajali kuwa watoto hao wanapaswa kuwa shuleni. Licha ya kukosa uhuru wa kuhudhuria masomo shuleni, watoto wanaoajiriwa huathiriwa kiafya kwani kazi wanazozifanya ni nzito kama nanga ilhali miili yao haijakomaa.

Watoto vile vile wana haki ya kuishi katika mazingira safi na kupata matibabu pale wanapokuwa wagonjwa. Mtoto anapogonjeka, anapaswa kupelekwa hospitalini ili atibiwe bali sio kufungiwa nyumbani kama mfungwa. Aidha, mtoto ana haki ya kupewa chakula na mavazi. Asipopewa haya, mtoto anaweza akahamia mitaani kutafuta usaidizi wa wasamaria wema, hivyo basi kuwa mtoto wa mtaani. Ni wazi kuwa watoto wakitimiziwa haki zao, watakua vyema na kujifaa maishani kwani wao ndio viongozi wa siku za halafu. Sharti sote tushirikiane katika kulitekeleza jambo hili kwani <u>kinga na kinga ndipo moto uwakapo</u>.

**41.** Ni kauli gani si sahihi kulingana na aya ya kwanza?
- A. Suala la kuwalinda watoto linapaswa kuchukuliwa kwa uzito
- B. Nchi nyingi duniani zinazingatia suala la haki za watoto
- C. Sheria zilizoundwa zimefanya dhuluma dhidi ya watoto kutupwa katika kaburi la sahau
- D. Mtu yeyote aliye na umri wa chini ya miaka kumi na minane ni mtoto

**42.** Haki ya mtoto ya kupata elimu hudhihirika wakati
- A. mtoto anapopelekwa shuleni
- B. mtoto anapopelekwa hospitalini
- C. mtoto anapofikisha umri wa miaka kumi na minane
- D. mtoto anapoishi katika mazingira safi

**43.** Jambo kuu linalowafanya watoto katika mataifa ambayo hayajaendelea kutopata elimu ni
- A. hali ya kutowajibika ya wavyele
- B. hali iliyokithiri ya ukata
- C. jamii kutoelewa haki za watoto
- D. ukosefu wa sheria za kuwalinda watoto

**44.** Kulingana na aya ya pili, ni dhahiri kuwa
- A. elimu ni tunu ya watu walio na vyao
- B. kuna usawa wa jinsi watoto wanavyopata elimu katika jamii
- C. watoto wengi kutoka jamii maskini huhusika katika shughuli za kutafuta riziki
- D. idadi kubwa ya watoto katika mataifa yanayoendelea imejiunga na shule

**45.** Kulingana na aya ya tatu, si kweli kuwa ubakaji
- A. umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika jamii
- B. huwavunjia watoto ubikira wao
- C. hutekelezwa na baadhi ya wanajamii
- D. huimarisha hadhi ya watoto

**46.** Maneno 'kula kalenda' katika taarifa yanamaanisha
- A. kufungwa jela
- B. kuadhibiwa vikali
- C. kukosa amani maishani
- D. kuaibisha mtu

**47.** Madhara yanayosababishwa na ajira ya watoto kwa mujibu wa kifungu hiki ni
- A. kuifanya miili ya watoto kukomaa
- B. kuwanyima watoto uhuru wa kupata elimu
- C. kuwahusisha watoto katika uchumaji wa riziki
- D. kuimarisha afya ya watoto

**48.** Ni ipi si haki ya watoto kwa mujibu wa kifungu hiki?
- A. Haki ya kupata ajira
- B. Haki ya kupata elimu
- C. Haki ya kupata matibabu
- D. Haki ya kupewa chakula

**49.** Methali 'kinga na kinga ndipo moto uwakapo' kama vile ilivyotimika katika taarifa inahimiza umuhimu wa
- A. ubaradhuli
- B. upendo
- C. ushirikiano
- D. uwajibikaji

**50.** Ni kichwa kipi kifaacho taarifa hii bora zaidi?
- A. Madhara ya ubakaji
- B. Ajira ya watoto
- C. Umuhimu wa elimu
- D. Haki za watoto